

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**MKUTANO WA NANE**

**YATOKANAYO NA KIKAO CHA SITA**

**12 SEPTEMBER, 2017**

## **MKUTANO WA NANE**

### **KIKAO CHA SITA TAREHE 12 SEPTEMBER, 2017**

#### **I. DUA:**

Mhe. Job Ndugai (Spika) alisoma Dua na kuongoza Kikao cha Bunge.

#### **Makatibu mezani:**

1. Ndugu Joshua Chamwela
2. Ndugu Lawrence Makigi

#### **II. KIAPO CHA UAMINIFU**

Mhe. Spika alimwapisha Mhe. Rehema Juma Migilla kuwa Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

#### **III. TAARIFA YA SPIKA**

Mhe. Spika alitoa taarifa ya Miswada iliyopitishwa na kusainiwa na Mhe. Rais kama ifuatavyo:-

- (1) Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi wa Mwaka 2017 (The Natural Wealth and Resources Contracts Review and Re-negotiation of Unconscionable Terms) Bill, 2017.
- (2) Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na umilii wa Maliasili wa Mwaka 2017 (The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Bill, 2017.
- (3) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya Mwaka 2017 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2017.

- (4) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2017).

Miswada hiyo sasa imepata kibali cha Rais na sasa kuwa Sheria za Nchi zinazoitwa:-

- (1) Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili Namba 5 ya Mwaka 2017 (The Natural Wealth and Resources Permanent Sovereignty) Act No. 5 of 2017).
- (2) Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi Namba 6 ya Mwaka 2017 (The Natural Wealth and Resources Contracts Review and Re-negotiation of Unconscionable Terms Act No. 6 of 2017).
- (3) Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 7 ya Mwaka 2017 (The Written (Miscellaneous Amendments) Act No. 7 of 2017).
- (4) Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 8 ya Mwaka 2017 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, No. 8 of 2017).

#### **IV. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

- (i) Mhe. Selemani Said Jafo aliwasilisha Mezani Maelezo kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2017 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2017).
- (ii) Mhe. Abdallah Shangazi aliwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Muswada huo.
- (iii) Mhe. Kasuku Samson Bilago aliwasilisha Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada huo.

## **V. MASWALI**

### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI)**

Maswali yafuatayo yaliulizwa:-

Swali Na. 67: Mhe. Daimu Iddy Mpakate

Nyongeza: Mhe. Daimu Iddy Mpakate

Swali Na. 68: Mhe. Lolesia Jeremiah Bukwimba

Nyongeza: Mhe. Lolesia Jeremiah Bukwimba

Swali Na. 69: Mhe. Ester Alexander Mahawe  
Mhe. Ester Alexander Mahawe

Swali Na. 70: Mhe. David Ernest Silinde

Nyongeza: Mhe. David Ernest Silinde  
Mhe. Abdallah Majula Bulembo

### **WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA**

Swali Na. 71: Mhe. Mattar Ali Salum

Nyongeza: Mhe. Mattar Ali Salum

### **WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Swali Na. 72: Mhe. Jaku Hashim Ayoub

Nyongeza: Mhe. Jaku Hashim Ayoub

## **WIZARA YA NISHATI NA MADINI**

Swali Na. 73: Mhe. Mwita Mwikwage Waitara

Nyongeza: Mhe. Mwita Mwikwage Waitara

Swali Na. 74: Mhe. Tunza Issa Malapo  
Mhe. Tunza Issa Malapo  
Mhe. Cecil David Mwambe

## **WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI**

Swali Na. 75: Mhe. Ahmed Juma Ngwali

Nyongeza: Mhe. Ahmed Juma Ngwali  
Mhe. Ally Saleh Ally

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

Swali Na. 76: Mhe. Kasuku Samson Bilago

Nyongeza: Mhe. Kasuku Samson Bilago  
Mhe. Masoud Abdallah Salum

## **WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

Swali Na. 77: Mhe. Ussi Salum Pondeza

Nyongeza: Mhe. Ussi Salum Pondeza

Swali Na. 78: Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia

Nyongeza: Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia  
Mhe. Khatib Said Haji  
Mhe. Nuru Awadh Bafadhili

## **WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI**

Swali Na. 79: Mhe. Jasson Samson Rweikiza

Nyongeza: Mhe. Jasson Samson Rweikiza  
Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete

Swali Na. 80: Mhe. Shally Josephat Raymond

Nyongeza: Mhe. Shally Josephat Raymond

Swali Na. 81: Mhe. Leonidas Tutubert Gama

Nyongeza: Mhe. Leonidas Tutubert Gama

## **VI. MATANGAZO**

- Kaimu Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni ni Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe.
- Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar Zubeir Ali Maulid yapo Speakers Gallery na Wajumbe wengine wa Baraza.
- Wageni wengine mbalimbali walitambulishwa.
- Mhe. Tundu Lissu anaendelea vizuri na Matibabu.

## **VII. MAAMUZI YA SPIKA**

Mhe. Spika alitoa Maamuzi yafuatayo:-

- (i) Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambayo imepewa kazi ya kujadili mambo yanayohusu Usalama wa Wabunge na Wananchi kwa ujumla imuite na kumhoji Mhe. Saed Ahmed Kubenea, kufuatia maneno yake aliyoyatoa kanisani tarehe 10/9/2017 ambayo yanaonyesha anao ufahamu zaidi kuhusiana na tukio la kushambuliwa kwa Mhe. Tundu Lissu.
- (ii) Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge imuite na kumhoji Mhe. Saed Ahmed Kubenea kwa kumtuhumu Spika kusema uongo Bungeni wakati akitangaza idadi ya risasi zilizopigwa kwenye gari ya Mhe. Tundu Lissu na hivyo alilidanganya Bunge. Mhe. Spika aliagiza kuwa Mhe. Kubenea atafutwe na kwenda kwenye Kamati hiyo ili athibitishwe maneno hayo.
- (iii) Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge imuite na kumhoji Mhe. Zitto Zuberi Kabwe kufuatia kauli zake alizozitoa kwenye Mitandao kwamba Mhimili wa Bunge umewekwa mfukoni na Serikali na kwamba Bunge limekosa kushughulikia Taarifa za Kamati mbili za Almasi na Tanzanite ambazo alidai zilitakiwa kuwasilishwa na kujadiliwa Bungeni.
- (iv) Maneno yaliyomo kwenye Hotumba ya Kambi ya Upinzani yanayosema Mhe. Spika ameridhia mabadiliko ya Uongozi wa CUF hapa Bungeni yafutwe kwa kuwa yeye hajaridhia chochote isipokuwa anatangaza tu kile anacholetewa na Vyama.

## **VIII. MIONGOZO**

- (i) Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda alitumia Kanuni ya 68(7) kuomba muongozo kwamba majibu ya nyongeza kwenye swali na. 70 hayakidhi na kuomba Serikali ifikirie kuzirudisha Serikalini baadhi ya Shule za umoja wa wazazi CCM zisizokuwa na wanafunzi.

- Mhe. Naibu Spika alitoa uamuzi kuwa muuliza swali la msingi ameridhika na pia muongozo hauombwi kwa majibu ya nyongeza kwa mbunge asiye mwenye swali.
- (ii) Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara aliomba muongozo na kuuliza kama Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama inashughulikia matukio ya Ulinzi na Usalama wa Nchi kwa ujumla au ni kw aWabunge tu. Aidha, alieleza kama Bunge linatambua Uongozi upi wa CUF hapa Bungeni na kwa nini Uongiz mpya uliotangazwa tarehe 11/9/2017 umepewa siti za mbele.
- Mhe. Naibu Spika aliahidi kutoa majibu baadae.
- (iii) Mhe. Mussa Bakar Mbarouk alitumia Kanuni ya 68(7) na kuuliza Serikali ina mpango gani kuhusu vitendo vya kubomoa nyumba za wananchi katika Vijiji vilivyopo karibu na Hifadhi.
- Mhe. Naibu Spika alieleza jambo hilo halijatokea Bungeni mapema.
- (iv) Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia alimpa Taarifa Mhe. Sophia Mwakagenda kuhusu uamuzi wa shule za Wazazi za CCM zilizoamuliwa kutoka au kubaki ndani ya Jumuiya.

## **IX. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2017 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2017*].

- Mwanasheria Mkuu wa Serikali alitoa maelezo ya Muswada na kutoa Hoja kwamba Muswada huo sasa usomwe mara ya Pili na kujadiliana na Bunge.
- Mhe. Mohammed Omary Mchengerwa aliwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kataiba na Sheria kuhusu Muswada huo.



- Mhe. Ally Saleh Ally aliwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhus Muswada huo.

Uchangiaji wa jumla ulianza kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Mwitwa Mwikwabe Waitara - CHADEMA
2. Mhe. Zuberi Mohammed Kuchauka - CUF
3. Mhe. Hamidu Hassani Bobali - CUF
4. Mhe. Joseph George Kakunda - CCM
5. Mhe. Dkt. Diodorus Buberwa Kamala - CCM
6. Mhe. Omary Tebweta Mgumba - CCM
7. Mhe. Isack Kamwelwe - CCM (NW – Maji)
8. Mhe. Prof. Joyce Ndalichako - CCM (W – EST)

Mtoa Hoja Mwanasheria Mkuu wa Serikali alipewa fursa ya kuhitimisha Hoja yake na kutoa ufafanuzi wa Hoja zilizotolewa wakati wa mjadala alitoa hoja na iliungwa mkono.

Bunge liliingia katika hatua ya Kamati ya Bunge Zima na kuanza kupitia Muswada Ibara kwa Ibara na kupitisha Muswada wote pamoja na marekebisho yaliyopendekezwa na Serikali.

Bunge lilirudia na Mtoa Hoja alitoa Taarifa ya Kazi ya Kamati, alitoa Hoja kwamba Bunge sasa likubali kupitisha Muswada huo, Bunge lilihojiwa na kupitisha Muswada.

Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2017 ulisomwa Mara ya Tatu na Naibu Spika alitangaza kwamba Muswada huo sasa umepitishwa rasmi na utapelekwa kwa Mhe. Rais kwa ajili ya kibali chake ili kuwa Sheria kamili.

## **X. KUAHIRISHA BUNGE**

Saa 7.15 Mchana Naibu Spika aliahirisha Bunge hadi tarehe 13/9/2017 saa 3.00 Asubuhi.